Ndoto na Njozi

Alhamisi, Machi 9, 2017

Utakatifu kwa Muumba wa Milele!

NDOTO NA NJOZI

na

Jeanine SAUTRON

KANISA LA PHILADELPHIA,

"MASALIO"

Wazishikao AMRI za MUNGU, ikiwemo SABATO YA SIKU YA SABA, yaani JUMAMOSI na IMANI ya YESU.

IMANI ya YESU:

ROHO WA UNABII.

---

(1) **ZILE PEPO ZIMEACHILIWA.**

Ndoto na Njozi

Sura ya 531, Njozi Namba 1

(2) Mataifa yafanya vita hapa duniani. YESU, mwana wa Mungu, vilevile afanya vita dhidi ya mataifa ya dunia. Mungu ndiye atakayeufunga mjadala katika jambo hili.

(3) **"Dunia ni yangu,"** YESU alisema.

(4) **"Mimi ndiye Mungu. Dunia ni yangu,"** YESU alisema.

(5) **"Dunia ni yangu,"** YESU alisema.

(6) **Yeye atayaangamiza mataifa yote.**

Hakuna atakayeponyoka!

(7) YESU yuaja kupambana na mataifa kwa upanga wake wenye sehemu mbili za makali utokao kinywani mwake. YESU asogea kama askari ili kuyazidi nguvu mataifa:

Muda wao umetamatishwa.

Huu ndio MWISHO!

NJOZI

(8) **Mungu afanya vita dhidi ya mataifa yote:** Njaa, ukame, dhoruba, tsunami, mitetemeko ya ardhi, ishara kila mahali nchini na hata angani: **Mungu ametangaza vita dhidi ya wakazi wa dunia. Muda wao umekwisha.**

(9) YESU alisema, **"Ile miaka elfu sita (6,000) imekamilika. Kizazi hiki cha umri wa miaka 45 hakitapita."**

(10) Niliingia kwenye njozi. Nikaliona jeshi la farasi weupe na waendeshaji wao wakienda shoti kwa kasi kuelekea kwangu.

(11) Mbele ya kikosi hiki kikubwa nilimwona farasi mweupe ambaye juu yake aliketi mtu aliyevaa taji ndefu kichwani.

(12) Nilitazama. Vazi lake lilikuwa nyekundu, yaani rangi ya damu. Jeshi hili lilikuwa likisafiri kwa kasi.

(13) Nilimtazama mtu huyo mwenye vazi nyekundu. Uso wake ulijaa hasira ya kutisha. Nikapiga yowe,

"Utukufu! Utukufu! Utukufu kwa yule Aishiye Milele!"

(14) Roho mtakatifu akanijia, ndipo nikapiga yowe tena: **"Utukufu! Utukufu! Utukufu!"**

(15) Nilitetemeka. Njozi ya ajabu hiyo! Jeshi hilo lilisogea kuelekea kwangu, ndipo nikamwona yule mtu mwenye lile vazi nyekundu, lililopakwa damu; sura ya uso wake ilikuwa ni ngumu kama jiwe. Niliihisi hasira iliyokuwa ndani yake. Niliuona upanga wenye sehemu mbili za makali ukitoka kinywani mwake.Nilihofia uhai wangu.

(16) Kikosi hicho kilichokuwa kikienda shoti kilisimama mbele yangu. Nilizingirwa na farasi hao weupe ambao walinizunguka kwa mviringo. Kisha yule aliyevaa nguo nyekundu akaja kuelekea kwangu kwa kasi mno, huku farasi wake akisimama ghafla mbele yangu. Alinitazama. Nami pia nikamtazama huku amelivaa taji lake lenye taji kadhaa kichwani, ambalo lilikuwa ni la kuvutia sana.

(17) Mrefu na adhimu, mwendeshaji huyu wa farasi – huku akiwa na vazi lake nyekundu – alilimatia, akawa akinizungukazunguka mara kadhaa *mbele ya kikosi chake*. Nilikuwa nikitetemeka.

(18) Askari huyu wa farasi aliliamrisha jeshi lake lifanye guaride kamilifu. Ndipo wakapangia vilivyo.

(19) Mwendesha farasi huyu mwenye vazi nyekundu lililopakwa damu alipita tena na tena, huku akienda shoti mbele ya kikosi chake, ndipo akawasili mbele yangu ghafla kwa kwenda shoti ya kasi. Nilimwona farasi huyo mkubwa, mweupe ajabu! Kisha mtu huyo mwenye vazi nyekundu lililopakwa damu akaja na kusimama huku akikabiliana nami.

(20) Nilimtazama, nikamwona mfalme mkuu mbele yangu, yaani mtawala, mfalme mkuu. Uso chini ya taji hiyo ndefu ulinitazama na kutabasamu. Yeye alikuwa juu ya farasi yake karibu nami, bila ya kunigusa.

(21) Lilisafiri kwa kasi, kasi sana. Lilionyesha nguvu za ajabu, yaani jeshi hili la mbinguni! Mwenye nguvu zaidi ni yule mtu aliyevalia nguo nyekundu, iliyopakwa damu, pamoja na farasi wake. Nilipendezwa na taji hilo ndefu ambalo juu yake kulikuweko na taji kadhaa zilizopambwa na mawe ya thamani. Uzuri ajabu!

(22) Nilikuwa katika njozi mbinguni. Katika njozi hiyo niliona nguvu za jeshi hilo. Nilikuwa nikitetemeka.

(23) Yule mtu mwenye nguo nyekundu alishuka toka juu ya farasi wake na kuliamrisha jeshi hilo lake liondoke. Katika njozi hii, mtu huyo mwenye nguo nyekundu alikuwa akisimama kando yangu. Nikaliona jeshi lake likiondoka juu ya farasi zao.

(24) Baadhi yao walitaka kusalia pamoja na mtu huyo na Jeanine, lakini aliwaambia, "Ningetaka kusalia na Jeanine pekee kwa njozi hizi." Pia alimwamuru farasi huyo wake ajiunge na wanajeshi hao waondoke pamoja.

(25) Nilimwona malaika wa zamu, mwenye mabawa yaliyokunjwa mgongoni, akija kwa mtu huyo aliyevalia nguo nyekundu na kumkabidhi kiti chake cha enzi cheupe. Ndipo akaketi juu yake.

(26) Mtu huyo aliniambia, **"Mimi ndiye YESU, mwama wa Mungu. Usiogope, Jeanine:**

Neema yangu yakutosha."

(27) Pale aliponiita "Jeanine," yaani jina langu la kwanza, nilijihisi salama. Sasa nilijua kuwa mtu huyo alikuwa YESU, mwana wa Mungu. Alikuwa bado amevalia nguo yake nyekundu na taji lenye vijitaji vya kupendeza. Nikajiambia, "Ni mfalme mkuu, mtawala."

(28) Malaika mhudumu alimvua vazi hilo nyekundu na kuiondoa taji hiyo yenye vijitaji iliyokuwa kichwani mwake. Kwa utaratibu alilikunja lile vazi lililopakwa damu na kuipanga ile taji kwa uangalifu.

Ndoto na Njozi
Sura ya 530 – 1, Njozi Namba 2
NJOZI

(1) Baada ya hayo, niliona kuwa kiti hicho kikuu cheupe cha enzi kiliwekwa na huyo malaika juu ya jukwaa kubwa, jeupe na lililotukuka.

(2) YESU alilipanda jukwaa hili na kuketi juu ya kiti hicho kikuu cheupe cha enzi. Niliona kuwa alikuwa pekupeku. Alikuwa ameketi kama **mfalme wa wafalme wa mifumo ya sayari.**

(3) Kisha alimwambia huyo malaika mhudumu aende hekaluni ayachukue makaa ya moto, aijaze chetezo kwa hayo, kisha amletee.

(4) Muda ulipita. Hatimaye nilimwona akiwasili na hiyo chetezo, akaiweka sakafuni, kando na hilo jukwaa.

(5) Niliitazama chetezo hii yenye kufukiza. Vilimi vya moto vilikuwa vikitoka ndani yake.

(6) YESU aliinuka toka kitini chake kikuu na cheupe cha enzi. Akamwongelesha baba yake na kusema:

"BABA....."

– Huku akiidhihirisha mikono yake iliyotobolewa, na kuonyesha alama zilizokuwa mikononi, na miguuni –

"BABA,

huu ndio mwisho wa saa. Wakati umefika wa kukomesha dhambi na mauti milele, kuzifuta toka kwenye mifumo ya sayari."

(7) **"Baba, damu yangu!**

Damu yangu! Damu yangu!

(8) YESU alikuwa akilia kwa sababu ya huo mwisho wa saa. Ile miaka 6,000 aliyopewa shetani imekamilika, imekwisha, imekwisha pamoja na dhambi na mauti, ambavyo havitakuwepo tena.

(9) **"Mauti,"** YESU alisema, **"hayatakuwepo tena. Kwani mshahara wa dhambi ni mauti. Mauti na dhambi havitakuwepo tena. Nitayafutilia mbali mauti toka kwenye mifumo ya sayari."**

(10) Alinipandisha juu ya jukwa hilo na kuniambia,

"Neema yangu yakutosha."

(11) Niliweza kufanya hivyo kwa roho wa YESU, ambaye alinifanya nisimame mbele zake.

(12) YESU alikuwa akinitazama. Niliyainamisha macho yangu. Kisha nikayainua macho yangu. Alikuwa bado amenikazia macho. Ndipo nikajiuliza swali hili, "Mbona yeye anikazia macho pasipo kusitisha? Singeuepuka huo mtazamo wake. Nilihisi kuwa alikuwa alikuwa akiyasoma yote yaliyokuwa moyoni mwangu na kuyafahamu yote yanayonihusu. Nilishawishika kuwa singebishana naye kuhusu lolote. Aliyafahamu yote kunihusu. Sikustahili kuwa juu ya jukwaa hili.

(13) Nilitaka kuondoka. Nilitazama nyuma yangu. Mimi sikustahili. Nilihisi kuwa **yeye ni Mungu, Mungu wa mifumo ya sayari.**

(14) YESU aliunyosha mkono wake kwangu na kuniambia, **"Wewe wastahili kuwa hapa; umepata neema machoni pangu."**

(15) Akaniambia, "Njoo karibu, njoo karibu, njoo

karibu nami, ee bi harusi wangu." – alipokuwa angali akiyasema hayo, nilijipata nikiwa karibu na YESU. –

"Neema yangu yakutosha."

(16) YESU aliniongelesha kuhusu **huyo bi harusi wake, yaani "masalio" wa Aishiye Milele huko Oregon.**

(17) Katika njozi, yeye alinifanya niondoke kuelekea Oregon. Tulikuwa pamoja kwenye njozi hii.

(18) Niliyaona maeneo mapana ya malisho mbele yangu. Hewa ilikuwa safi, ikawa ikipita usoni mwangu kama vile upepo mwanana wa magharibi. Katika njozi, niligundua pahali hapa: **OREGON**.

(19) YESU aliniambia, **"Niko Oregon pamoja nawe. Hapa ndipo penye hifadhi ya 'masalio', yaani mke wangu. Nitautuma upepo ili uzipeperushe tauni za miji mikuu mbali na hapa. Nitaifagilia mbali ile salfa, moshi na pia moto. Nitaisafisha kwa pumzi ya kinywa changu."**

Ndoto na Njozi
Sura ya 531, Njozi Namba 3

(1) Nilirudi toka kwenye njozi, kisha nikaingia kwenye njozi tena pamoja na YESU, huku nikisimama kando yake juu ya lile jukwaa jeupe la utukufu. YESU aliifungua mbingu ili niweze kuitazama dunia.

(2) Ilikuwa ni usiku. Niliona jiji kubwa lililong'aa sana, likisogea machoni pangu. Niliyaona maghorofa marefu, yaani minara iliyopaa juu angani nusura kuligusa mbingu. Mji huu uling'aa kwa taa. Niliziona taa hizo kwenye madirisha mengi yasiyohesabika.

(3) YESU alimwambia yule malaika mhudumu atwae chetezo iliyojaa makaa ya moto, ambayo ilikuwa ikitoa moto, na kuirusha duniani kwa nguvu zake zote. Naye akatenda jinsi alivyoagizwa na Yesu.

(4) Katika njozi niliona, kufumba na kufumbua, kuwa mji huo mkuu, ambao minara na maghorofa yake yaling'aa sana, uliupoteza huo mwanga wake ghafla. Mji huo mkuu ulikumbwa na giza totoro. Hakuna chochote tena. Hakuna mwangaza tena. Ni giza totoro tu. Usiku wa giza.

(5) Kutoka pahali nilipokuwa pamoja na YESU, yaani juu ya jukwaa, singethubutu kubanduka, kwani nilihofia kuuchungulia huo utupu uliokuwa mbele yangu.

(6) YESU aliniambia, "Ile baraghumu ya sita (6) ni ya kutisha kuliko yale utakayoyaona katika njozi hii. Mji huu uliouona ni **New York**, yaani makao makuu ya biashara Marekani. Utafunikwa na giza mchana na usiku. **Miji mikuu, pamoja na minara na maghorofa yao itatumbukia gizani.** Watavipoteza vyote walivyojivunia duniani. Maghorofa na minara yao itaporomoka kama vitita vya mabua."

(7) YESU aliniambia kuwa yeye afanya vita dhidi ya mataifa.

(8) Malaika mhudumu pia alinifichulia haya mbele ya YESU: "Ile baraghumu ya sita (6) ni ya kutisha kuliko makaa haya ya moto yaliyotumwa duniani." – Nilitetemeka.

(9) YESU aliniambia:

"Neema yangu yakutosha."

(10) YESU aliniambia: **"Nakutuma tena katika njozi hadi kwenye hayo makao makuu ya biashara Marekani: New York. Awali ulikuwa katika njozi huko New York."**

(11) Niliacha kumwona YESU. Nilikuwa huko New York, kama ionekanavyo toka mbinguni. Niliuona mji huu mkuu mbele ya macho yangu.

(12) Majira ya usiku singeweza kuipata taswira kamili ya New York, kwani nilichokiona ni taa tu zilizosababisha kung'aa kwake. Lakini nilipoutazama mchana, nilipata kuwa New York ni tofauti na jinsi nilivyouona usiku. Nilisikitika. Nilichokiona ni saruji tupu, saruji iliyoinuka toka kwenye minara hii, yaani maghorofa haya, hadi mbinguni.

(13) YESU aliniachia muda ili niutazame mji huu mkuu wa Marekani, ambao niliupata saa za mchana. Nilikuwa nikiutazama. Nikastaajabu. Niliufurahia mji huu wa New York. Niliinamisha kichwa changu kidogo, bila kuitambua hatari iliyokuwepo. – YESU aliniambia, **"Usiinamishe kichwa chako sana; kuna hatari ya kutiwa kizunguzunguna na hatimaye kuzirai."**

(14) Katika njozi hii, nilikawia, huku nikiutazama mji wa New York jinsi unavyoonekana toka mbinguni. Nao ulikuwa mbele ya macho yangu. Ilikuwa shani ajabu machoni pangu! Lakini nilipotazama kwa makini zaidi, nilitambua kwa mshangao, kuwa hapakuwepo tena mitaa, wala taa za barabarani, wala mwangaza, wala watu wowote huko chini. Nikajiuliza swali, "Kwani walienda wapi?"

(15) Ndipo macho yangu yakatazama chini zaidi. Nikauona mji huo wa New York, yaani makao makuu ya biashara Marekani, ukiwa umezama ndani ya

maji. Niligundua kuwa maji hayo yalikuwa yakipanda na kupanda. Maji yalikuwa karibu kufikia upeo wa minara na maghorofa hayo.

(16) Niliisikia migumio iliyotoka kwenye minara na maghorofa hayo. Watu walikuwa wakifariki. Walikuwa wamenaswa na hayo maji yaliyopaa kwa kasi wakati wa usiku, bila kuwaachia nafasi wakazi wa New York kuhama kutoka kwenye minara hiyo na maghorofa hayo.

(17) New York, ambayo ndiyo makao makuu ya biashara, ilikuwa imefunikwa na mawimbi kabisa. Nilivisikia vishindo vya kupasuka kwa hiyo minara na maghorofa, vilivyotangaza kuporomoka kwa majengo hayo. Nilikuwa nikitetemeka. Wakazi walinaswa wakiwa bado wangali wamelala.

(18) Niligundua kuwa siku ilikuwa yapambazuka. Ilikuwa asubuhi. Mitaani mwa jiji hili kuu, niliziona mashua zilizowabeba watu ambao waliizunguka minara hiyo na maghorofa huku wakiwatafuta manusura kwenye madirisha. Hakukuwa na kelele zozote. Mara kwa mara sauti ya mgumio ilisikika ikitoka ndani ya minara hiyo mikuu.

(19) Niliona kuwa wale waliokuwa ndani ya hizo mashua hawangeweza kufanya chochote. Niliwaona waokoaji. Hawangeweza kuyafikia madirisha ya minara hiyo na maghorofa hayo.

(20) Nilifunuliwa kuwa yale mabaya zaidi yalikuwa yangali bado kutendeka. Minara hii, kwa sababu ya huo mbano wa maji yanayoizingira, ingezama jinsi meli inavyozama baharini, huku mbano huo wa maji ukifikia karibu kila ngazi ya maghorofa hayo. Maji yalikuwa yamepaa hadi karibu kila ngazi ya minara mirefu zaidi.

(21) YESU afunua:

TAUNI
YA MIJI MIKUU

itapaa hadi mbinguni. Tauni ya baharini, ya ardhini na ya majini itapaa hadi juu mbinguni.

(22) Ilikuwa karibu usiku. Nilikuwa nikizitazama mashua hizo zilizotapakaa kote New York, ndipo nikajihisi mgonjwa. Harufu ya salfa, tauni kali, yaani gesi, ilinizuilia kupumua. Ndipo YESU akanirudisha karibu naye kutoka kwenye njozi hiyo.

(23) Nilikuwa karibu naye sasa. Akaniambia, **"Ulikuwa umechanganyikiwa. Ulikuwa karibu kuzirai."**

(24) Yule malaika mhudumu aliniambia, "Ulikuwa karibu kuzirai. **Yule malaika wa baraghumu ya sita (6) atakuwa ni wa kutisha kuliko hiyo tauni ambayo umeiona na kuihisi."**

(25) Yesu aliniambia, "Hiyo ilikuwa ni harufu ya salfa. Tauni hii ilikuwa ni kama vile salfa. Ungekuwa tayari umekwisha fariki. Gesi zitaichafua dunia."

(26) Njozi hiyo ya New York yaishia hapa na hiyo tauni. Katika njozi hiyo niliona sura ya kuhuzunisha ya New York: yaani saruji tupu, saruji iliyozama majini.

(27) Nilifahamishwa, kuwa wanadamu hawakuumbwa ili waishi ndani ya maghorofa haya, minara hii, ambacho ndicho kiburi cha mataifa duniani. Kiburi hiki kitaangamizwa na mwana wa Mungu.

(28) Hivi karibuni vitu hivi havitakuwepo tena. **YESU amefichua katika Njoto na Njozi ya kuwa miji mikuu itaporomoka kwa kuzama majini, yaani miji ya Sodoma na Gomora:**

Hakuna atakayeponyoka!
iko karibu sana!

(29) Tauni, mikurupuko ya maradhi, itajaa duniani.

Ndoto na Njozi

Sura ya 531, Njozi Namba 4

NJOZI

(1) **IKO KARIBU SANA.**

(2) Makaa ya moto kutoka ndani ya chetezo, yaliyorushwa toka mbinguni, yanateketeza kila kitu duniani. "**Dunia nzima *itaathirika. Hakuna sehemu hata moja* itakayoponyoka,"** YESU akasema.

NJOZI

(3) Niliona kuwa makaa hayo yanayowaka, mekundu kwa moto, yametapakaa juu ya vilele barafu, juu ya mito, kila mahali duniani. Wala hayatoki. Ni ya kiungu.

(4) YESU, mwana wa Mungu, afanya vita na mataifa yote ya dunia:

Ilitimua mbio!
Hakuna atakayeponyoka!

(5) Nilimwona Yesu akilia kwa ajili ya vyote alivyoviumba na ambavyo sasa vyaangamia.

(6) Nimefahamishwa: uharibifu huu wa dhambi na kifo utafuatwa na dunia nyingine mpya, yenye kupendeza hata zaidi, ambapo ndani yake hakutakuwepo tena uovu, wala kifo na mateso yake.

(7) YESU, mwana wa Mungu, aiharibu dunia hii ili aumbe ulimwengu mpya wenye kupendeza zaidi. YESU ndiye aliyenifichulia mpango huu.

Huu ndio mwisho
wa saa.

(8) **BARAGHUMU YA SITA**
ITAKUWA YA KUTISHA ZAIDI
YA YALE MAKAA YA MOTO
YALIYOTUMWA DUNIANI.

Ndoto na Njozi
Sura ya 531, Njozi Namba 5
NJOZI

(1) Katika njozi hii nilimwona YESU akiandamana na jeshi lake juu ya hivyo vilele barafu, yaani mito mikuu ya barafu duniani.

(2) Nilikuwa pamoja na YESU juu ya kilele barafu cha Greenland, pia kwenye mto mkubwa wa barafu. Jeshi hilo lake lilikuwa pamoja naye juu ya wingi huu wa barafu, huku wakimwandama.

(3) Niliviona vibonge hivi vya barafu vikijitenga. Kulikuweko mto uliovitenganisha vibonge hivyo viwili vya barafu. YESU alinipeleka hadi mahali hapo.

(4) YESU aliniambia,

"Hii ni ghadhabu ya Mungu."

(5) **"Mimi nafanya vita dhidi ya mataifa,"** YESU akasema. **"Imetosha kwa waovu.**

Huu ndio mwisho wa saa."

(6) Nilikuwa nikitembea kando ya YESU. Ilikuwepo mito ya barafu tu. Nilikuwa pekupeku, nalo vazi langu lilikuwa jeupe kama theluji. Niliacha kumwona YESU.

(7) Niliwaona wapanda farasi juu ya farasi wao weupe wakitembea karibu nami. Macho yao yalikuwa juu yangu; yaani walikuwa wakinitazama.

(8) Walikuwa wapendeza! – Njozi ya ajabu hiyo! – Wote walivalia nguo nyeupe katika njozi hii: yaani wapanda farasi na farasi wao, Jeanine na vazi lake nyeupe, na YESU. Kila kitu kilikuwa ni cheupe, cheupe kuliko hiyo mito ya barafu.

(9) Mara nikayaona makaa juu ya hiyo barafu. – YESU akaniambia, **"Wewe, usiyaguse hayo. Ghadhabu iko ndani ya makaa haya,"** – makaa hayo yaliyorushwa duniani, yaotoka ndani ya chetezo ya YESU, yaitumbukiza dunia kwenye misukosuko, uchungu na mauti.

(10) YESU afanya vita dhidi ya mataifa. Miji mikuu ya dhambi itazama majini. Mito ya barafu yayeyuka. Dunia itafurika pande zote. Zitakuwepo tsunami na mitetemeko ya ardhi yenye uwezo mkubwa. Makaa haya, popote yanapopatikana, hupelekea mito kufurika kwa uwezo mkubwa, hivyo kusababisha miporomoko ya ardhi. Hulitikisa gamba la dunia.

(11) **"Magma ya volkano fulani yachemka ndani ya dunia,"** YESU akasema, **"yaelekea kulipuka."** – Niliuona ulingo wa moto duniani. Gamba la dunia latikisika.

(12) YESU alinionyesha, kufuatia joto kali litokanalo na kuongezeka kwa magma, ya kuwa gamba la dunia sasa latikisika, hivyo kusababisha tsunami na mitetemeko ya ardhi. **"Volkano zitaamka,"** YESU alisema, **"juu ya huo ulingo wote wa moto, yaani ulingo wote wa moto uzungukao dunia nzima."**

(13) Makaa hayo ya moto kutoka ndani ya chetezo ni moto ambao hauzimiki. Makaa haya hayatazimwa; ni ya kiungu. Yametawanywa duniani ili kuwatumbukiza watu kwenye misukosuko.

(14) YESU alisema**, "Baragumu ya malaika wa sita (6) itakuwa ya kutisha! Hata hivyo wanadamu hawatatubu dhambi zao. Waovu watazidi kuwa waovu."** – Ndiyo sababu YESU aliamua kuitamatisha dunia hii ya dhambi, mateso na mauti.

(15) Ni kwa mujibu wa wenye haki ambapo YESU atakuja kuikomesha dunia hii ya dhambi. Mauti hayatakuwepo tena.

(16) Ni hayo makaa ya moto ambayo yanaliharibu gamba la dunia. Yanalenga kuitumbukiza dunia ndani ya maji yanayopanda na kuifurikisha mito, hivyo kuiangamiza miungu, walimwengu, wanaosherehekea, na miji mikuu ya Sodoma na Gomora:

Hakuna atakayeponyoka!
Yesu ametangaza:
Hakuna atakayeponyoka!
Huu ndio MWISHO wa saa.

(17) **"Moto, salfa na moshi,"** YESU aliniambia, **"Ile baragumu ya sita (6) i karibu. Baada ya makaa ya moto, wakazi wa dunia watakuwa chini ya baragumu ya sita. I karibu. Baada ya makaa ya moto, baragumu ya sita (6) itakuwa na athari zake duniani, kuitumbukiza dunia kwenye maafa mabaya zaidi."**

(18) **"Huu ndio MWISHO wa ulimwengu,"** YESU aliniambia.

"Yote yamekaribia sana!"

(19) **Zile pepo nne (4) zimeachiliwa** kwa muda kiasi sasa. Yote yataenda kwa kasi, nayo matukio yataachiliwa moja baada ya nyingine.

(20) **"Shikilia taji yako,"** YESU aliniambia.

(21) Baragumu ya sita iko karibu. **YESU alitoa ujumbe huu kwa walio wake na kwa walimwengu:**

(22) **"Songamaneni! Songamaneni!"**

(23) **"Shikilia sana taji yako!"**

Jeanine Sautron